



Tanzania Cigarette Public Limited Company
Rasilimali ya Tanzania



**CREATING
FULFILLING
MOMENTS.**

**CREATING
A BETTER
FUTURE.**

TCC Plc Integrated
Report 2023



Content Yaliyomo



Executive Summary Muhtasari wa Jumla

TCC Plc at a Glance Muhtasari wa TCC Plc

- 08 Purpose, Vision and Management Principles
- 09 Dhumuni, Dira na Kanuni za Usimamizi
- 10 Brief History
- 11 Historia Fupi
- 12 The TCC Plc Value Chain
- 13 Mnyororo wa Thamani wa TCC Plc
- 14 Product Portfolio
- 14 Orodha ya Bidhaa
- 16 Performance Review
- 17 Uhakiki wa Utendaji
- 18 Key Performance Indicators
- 20 Viashiria Muhimu vya Utendaji
- 22 Members of the Board
- 22 Wajumbe wa Bodi
- 26 Management Team
- 26 Timu ya Usimamizi




Message to Stakeholders Ujumbe kwa Wadau

- 28 Message from the Chairman
- 30 Ujumbe kutoka kwa Mwenyekiti
- 32 Message from the CEO
- 34 Ujumbe kutoka kwa Afisa Mtendaji Mkuu

ESG Priorities and Materiality Topic Reporting for 2023 Vipaumbele vya ESG na Ripoti ya Nyanja Muhimu kwa 2023

- 37 Material Topic Identification and Sustainability Goals
- 39 Materiality Analysis and Progress towards Sustainability Goals
- 39 Governance
- 42 Environmental
- 44 Social
- 46 Utambuzi wa Nyanja Muhimu na Malengo Endelevu
- 48 Uchambuzi wa Nyanja na Hatua kuelekea Malengo Endelevu
- 48 Utawala
- 51 Mazingira
- 53 Jamii



Annual Report and Audited Financial Statements

- 57 Corporate Information
- 58 Report by Those Charged with Governance
- 73 Statement of Directors' Responsibilities
- 74 Declaration by the Head of Finance
- 76 Independent Auditor's Report
- 80 Financial Statements
 - 80 Statement of profit or loss and other Comprehensive Income
 - 81 Statement of financial Position
 - 82 Statement of changes in Equity
 - 83 Statement of Cash Flow
 - 84 Notes to the Financial Statements

Appendix I - GRI Compliance

- 114 GRI Index
- 118 GRI External Assurance Letter



Disclaimer

The reporting period for this report covers January 1, 2023 to December 31, 2023.

This is an integrated report which covers all necessary annual reporting and Environmental, Social, and Governance (ESG) reporting requirements as per Global Reporting Initiative (GRI) 2021 and Tanzania Financial Reporting Standard (TFRS) 1 standards.

Tanzania Cigarette Public Limited Company (TCC Plc) overall ESG agenda, unless stated otherwise, aligns with the Tobacco Business Sustainability Targets, as of December 2023. Activities throughout the Company's operation are aligned to the metrics that are considered most material to the business and stakeholders. TCC Plc has focused its ESG agenda on the areas where the Company can make the most significant positive impact. Unless otherwise specified, the scope of this report covers the TCC Plc operations only.

Precautionary Principal Statement

TCC Plc confirms that the precautionary principle is adopted, meaning that where there are threats of serious or irreversible damage, lack of full scientific certainty shall not be used as a reason by the Company for postponing cost-effective measures to prevent environmental degradation or negative social effects.

Claim of Reporting in Accordance or in Reference to the GRI Standards

This report has been prepared in reference to the Core Option of the GRI 2021 Standards.

¹ In all incidences this report refers to "The Company" the report refers to TCC Plc

Tamko

Ripoti hii inalenga inatoa taarifa ya kipindi cha kuanzia Januari 1, 2023 hadi Desemba 31, 2023.

Ripoti hii jumuihi inatoa taarifa za mahitaji yote muhimu ya ripoti ya kila mwaka na mahitaji ya ripoti ya kimazingira, kijamii na kiutawala (ESG) kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Utoaji Ripoti wa Taasisi ya (GRI) 2021 pamoja na matakwa ya utoaji wa ripoti za mahesabu na matumizi ya kitaifa (TFRS) 1.

Ajenda jumuihi za kampuni ya Sigara (TCC Plc) za ESG zinajilekeza sambamba na malengo ya kudumu ya biashara ya Tumbaku ya Desemba 2023. Shughuli zote za kampuni hulinanishwa na viashiria ambavyo vinachukuliwa kuwa nyenzo ya taarifa kwa biashara na wadau. TCC Plc imeelekeza ajenda zake za ESG kwenye maeneo ambayo Kampuni inaweza kuleta matokeo chanya zaidi, isipokuwa ikiwa imebainishwa vinginevyo, ripoti hii enahusu shughuli za kiutendaji wa Kampuni ya TCC Plc pekee.

Tamko la Msingi la Tahadhari

TCC Plc inathibitisha kwamba tamko la tahadhari limepitishwa na Kampuni, ikimaanisha kuwa pale ambapo kuna tishio la uharibifu mkubwa au hali ya kutokuweza kurekebisha, kutokuwepo kwa taarifa kamili za kisayansi havitatumika kama sababu ya kuahirisha hatua za kuzuia uharibifu wa mazingira au athari hasi za kijamii.

Haki ya Kuripoti kwa Mujibu au Marejeleo ya Viwango vya GRI Ripoti hii imeandaliwa kwa kurejelea Misingi ya Viwango vya taasisi ya kimataifa ya utoaji wa ripoti wa GRI 2021.

¹ Neno "Kampuni", linamaanisha TCC Plc katika maeneo yote ya ripoti hii.

Executive Summary

TCC Plc's overarching purpose, "Creating Fulfilling Moments. Creating a Better Future.", is not just a statement but a guiding principle at the heart of all its endeavors. This ethos directs the Company's strategies, shapes its brand and culture, and defines its very existence. Committed to enhancing consumer experiences and contributing positively to society, TCC Plc focuses on anticipating consumer needs, creating superior stakeholder experiences, and delivering pleasurable moments. Despite facing challenges such as increased excise duties impacting operating margins, TCC Plc remains dedicated to innovation and diversification to lead the industry in total product experience and value delivery.

In 2023, the Company's net revenue increased by 9.7% compared to 2022. The increase is driven by a more than 10% growth in sales volumes, with contribution from both domestic and export segments. Despite a significant increase in excise duties, the Company still managed to deliver a positive growth in gross profit by 6.9% and maintain a stable net profit for year. Furthermore, the Company declared a total dividend per share for 2023 of TZS 500 subject to adoption by shareholders at the Annual General Meeting.

In its commitment to sustainability, TCC Plc pursues ambitious goals such as becoming carbon neutral by 2030 and achieving net-zero greenhouse gas emissions by 2050. The company actively reduces energy consumption, water use, and waste generation while investing in community

initiatives focused on economic empowerment, education for older youth, and environmental conservation.

TCC Plc places a high emphasis on its employment culture, ensuring fair compensation, talent development, and a supportive work environment. With initiatives like Collective Bargain Agreement, incentive programs, and regular employee engagement surveys, the Company fosters a positive workplace atmosphere. Additionally, TCC Plc has a strong consumer-centricity which is manifested in its promise to produce quality products and is committed to grow its profits to ensure competitive returns to its shareholders.

The Company maintains a strong stance against corruption, adhering strictly to anti-corruption policies and promoting ethical conduct among its employees.

Looking forward to 2024, TCC Plc remains optimistic about its business outlook despite global economic uncertainties. Considering Tanzania's positive GDP and inflation projections and TCC Plc's solid strategy and proactive approach the Company is poised to navigate challenges and seize opportunities. This approach will ensure the Company's continued success in the years to come through strong stakeholder engagement that effectively nurtures the interests of valued consumers, shareholders, employees and the society at large.

FINANCIAL PERFORMANCE 2023: 9.7% Revenue Increase

SUSTAINABILITY Carbon Neutral by 2030, Net-Zero Emissions by 2050

STAKEHOLDER FOCUS Talent Development, Consumer-Centricity, Community Investment, Competitive Returns

ETHICAL STANCE Strong Anti-Corruption Policies

2024 OUTLOOK Optimistic for 2024 despite Global Uncertainties Focus on Stakeholder Engagement



EXECUTIVE SUMMARY MUHTASARI WA JUMLA

Muhtasari wa Jumla

Dhumuni la TCC Plc ni "Kutengeneza Nyakati za Furaha. Kutengeneza Kesho iliyo Bora Zaidi." si kauli mbiu tu bali ni kanuni inayoongoza kiini cha jitihada zote za Kampuni. Dhumuni hili linaongoza mikakati ya kampuni, linaboresha chapa ya kampuni na utamaduni wake, na kuelezea maana kuu ya uwepo wake. Ikiwa imejielekeza kuimarisha uzoefu wa watumiaji na kuchangia matokeo chanya katika jamii, TCC Plc inazingatia na kulenga mahitaji ya watumiaji, kuboresha uzoefu na uridhishwaji wa wadau, na kuleta nyakati za furaha. Licha ya kukabiliwa na changamoto kama vile ongezeko la ushuru wa bidhaa ambao unaathiri gharama za uendeshaji, TCC Plc inaendelea kujidhatiti katika ubunifu na anuai ili kuongoza sekta katika utoaji wa bidhaa na huduma zenye thamani.

Mwaka 2023, pato halisi la kampuni liliongezeka kwa 9.7% ukilinganisha na mwaka 2022. Ongezeko hili lilichangiwa na ukuaji wa zaidi ya 10% ya mauzo ya jumla kwenye masoko ya nje na ndani. Pamoja na ongezeko kwenye viwango vya kodi ya ushuru wa forodha, Kampuni bado ilifanikiwa kupata ongezeko la pato ghafi kwa 6.9% na kuendelea kupata faida kwa mwaka. Zaidi ya hayo, Kampuni ilitangaza gawio la jumla kwa hisa kwa mwaka 2023 la TZS 500 baada ya kuidhinishwa na kupitishwa na wanahisa kwenye Mkutano mkuu.

Kupitia wajibu uliyojiwekea katika muktadha wa maendeleo endelevu, TCC Plc inafuata malengo makubwa kama vile kufikia usawa unaohitajika wa hewa ukaa ifikapo 2030 na kufikia kiwango sifuri cha uzalishaji wa gesi chafuzi ifikapo 2050. Kampuni inapunguza matumizi

ya nishati, maji, na uzalishaji taka huku ikiwekeza katika mipango ya jamii inayolenga uwezeshaji wa kiuchumi, elimu kwa vijana wakubwa, na uhifadhi wa mazingira.

TCC Plc imeweka mkazo mkubwa kwenye utamaduni wake wa ajira, ikihakikisha malipo ya haki, kuendeleza vipaji, na kuboresha mazingira ya kazi. Kupitia mipango kama Mkataba wa Hali Bora za Wafanyakazi, programu za motisha, na tafiti za mara kwa mara za ushirikishwaji wa wafanyakazi, Kampuni inaendelea mazingira chanya mahali pa kazi. Zaidi ya hayo, TCC Plc imejielekeza kumjali mteja, mwelekeo unaotajwa katika ahadi yake ya kuzalisha bidhaa bora na kujali makatwa ya mteja nakupitia hili kampuni imeazimia kuongeza faida zake ili kuhakikisha marejesho ya ushindani yenye tija kwa wanahisa wake.

Kampuni ina msimamo mkali dhidi ya rushwa, ikifuata kwa umakini sera za kupinga rushwa na kukuza mwenendo wa kimaadili miongoni mwa wafanyakazi wake.

Kuelekea 2024, TCC Plc inaendelea kuwa na mtazamo chanya kuhusu mwelekeo wa biashara yake licha ya changamoto za uchumi wa dunia. Kwa kuzingatia makadirio chanya ya Pato la Taifa na mfumuko wa bei nchini Tanzania, Kampuni inajielekeza kukabiliana na changamoto na kuchangamkia fursa zilizopo, ili kuhakikisha muendeleo wa mafanikio yake kwa miaka ijayo kupitia ushirikishaji thabiti wa wadau ambao unakuza kikamilifu maslahi ya watumiaji wake wanahisa, wafanyakazi na jamii kwa ujumla.

UTENDAJI WA KIFEDHA:
2023: Ongezeko la mapato kwa asilimia 9.7

UENDELEVU:
Hali ya kuttoa hewa ukaa ifikapo 2030, kutokuzalishaji wa hewa kabisa ifikapo 2050

MALENGO KWA WADAU:
Kuendeleza vipaji, kuzungatia mahitaji ya wateja, uwekezaji katika jamii, ushindani wenyenye tija

MSIMAMO WA KIMAADILI:
Sera madhubuti dhidi ya rushwa

MTAZAMO WA 2024:
Licha ya kutokuwa na uhakika duniani matarajio kwa 2024 mkazo katika ushirikishwaji wa wadau



02

TCC PLC AT A GLANCE MUHTASARI WA TCC PLC

Purpose, Vision and Management Principles

Purpose

“Creating Fulfilling Moments. Creating a Better Future.” is TCC Plc’s purpose. It is the Company’s North Star and is at the heart of everything the company does and how it is done. It guides TCC Plc’s strategies and ambition. It shapes the company’s brand and culture and is the reason for the company’s very existence.

TCC Plc is committed to creating a better future in which consumers everywhere can enhance their enjoyment of the Company’s products. TCC Plc is focused on anticipating consumer wants and needs, creating superior products and delivering pleasurable moments. This care is based on deeply felt Company values, and through a profound commitment to wider society. By innovating and diversifying TCC Plc’s product portfolio, the Company can ultimately lead the industry in total product experience and deliver greater value.

Vision

TCC Plc’s vision is to continue to be the number one tobacco Company in Tanzania.


Management Principles

Under the 4S model, TCC Plc strives to fulfill the Company’s responsibilities to its valued consumers, shareholders, employees and the wider society, carefully considering the respective interests of these four key stakeholder groups and exceeding their expectations wherever the Company can.

Consumers

The Company provides exceptional products and services that deliver value beyond fulfillment of diverse needs and preferences. To keep doing so, TCC Plc will upgrade its innovation capabilities by leveraging the JT Group’s diversity.

Shareholders



TCC Plc aims to enhance shareholder returns by delivering medium- and long-term profit growth, prioritizing whilst striking a balance between profit growth through business investments and shareholder returns.

Employees

TCC Plc aims to be an appealing, highly esteemed Company for which its employees are proud to work. While evaluating employees fairly and transparently and supporting their personal growth, the Company aims to foster a corporate culture that respects and embraces diverse values.

Society

To fulfill the Company’s responsibility as a member of society and contribute to the sustainable development of society through the business, TCC Plc will work with a wide range of stakeholders and strive to resolve various issues together.

The breakdown of the shareholders is outlined in the corporate information (page 57), further a stakeholder map as well as the respective engagement strategies are detailed in the Report by Those charged with Governance (page 63).

Dhumuni, Dira na Kanuni za Usimamizi

Dhumuni

“Kutengeneza Nyakati za Furaha. Kutengeneza Kesho iliyo Bora Zaidi.” ndio dhumuni la TCC Plc. Dhumuni hili ni muongoza njia na kiini cha kila kitu ambacho kampuni hufanya na jinsi kinavyofanywa. Dhumuni hili huongoza mikakati na matarajio ya TCC Plc. Pia, linatengeneza chapa na utamaduni wa kampuni na ndiyo sababu ya uwepo kwa Kampuni.

TCC Plc imeazimia kujenga mustakabali bora ambapo watumiaji kila mahali wanaweza kufurahia bidhaa ambazo Kampuni inazalisha. TCC Plc imezingatia mahitaji ya watumiaji kwa kutengeneza bidhaa bora zaidi, na zenye kuleta furaha. Kujali matakwa ya wateja kunatokana na namna Kampuni inathamini tunu zake, pia kupitia wajibu iliyojiwekea kwa jamii. Kwa kubuni na kutanua wigo wa bidhaa za TCC Plc, Kampuni itaongoza sekta kwa wateja kupata uzoefu wa bidhaa bora kwa kuzalisha bidhaa zenye thamani bora zaidi.

Dira


Dira ya TCC Plc ni kuendelea kuwa Kampuni namba moja ya bidhaa za tumbaku Tanzania.

Kanuni za Usimamizi

Kupitia muundo wa Kampuni wa 4S, TCC Plc inajitahidi kutimiza wajibu wa Kampuni kwa watumiaji wa bidhaa zake, wanahisa, wafanyakazi na jamii kwa ujumla, kwa kuzingatia kwa umakini mkubwa maslahi ya makundi haya manne muhimu ya wadau na kutimiza zaidi matarajio yao pale inapowezekana.

Watumiaji

Kampuni inatoa bidhaa na huduma bora zenye kutimiza mahitaji na matakwa mbalimbali ya watumiaji wake. Ili kuendelea kufanya hivyo, TCC Plc itaendelea kuimarisha uwezo wake wa kiubunifu ili kuendana na mahitaji mbalimbali kwa kuzingatia uwezo wa JT Group kwenye bidhaa na huduma inazotoa.



Wanahisa

TCC Plc inalenga kuongeza ukuaji wa pato la wanahisa kwa kuwahakikishia faida ya kati na ya muda mrefu, kwa kuweka kipaumbele na kuleta usawa kati ya ukuaji wa faida kupitia uwekezaji wa biashara na mapato ya wanahisa

Wafanyakazi


TCC Plc inalenga kuendelea kuwa Kampuni yenye mvuto na heshima kubwa ambayo wafanyakazi wake wanajivunia kufanya kazi. Kampuni inalenga kukuza utamaduni wake unaothamini na kuenzi thamani ya wafanyakazi huku ikiendelea kutathimini kwa usawa na uwazi kuwasaidia wafanyakazi kukua katika kazi na katika nyanja binafsi.

Jamii

Kampuni inawajibika kama mwana jamii katika uchangiaji wa maendeleo endelevu ya jamii kupitia biashara, TCC Plc itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali na kujitahidi kutatua masuala mbalimbali kwa pamoja.

Mgawanyo wa wanahisa umetajwa katika sehemu ya taarifa za Kampuni (ukurasa 57), pia orodha ya wadau kwa kuzingatia mahusiano yao na kampuni imeelezwa kupitia ripoti ya wakurugenzi (ukurasa 63).

Brief History



Brief History

TCC Plc, a member of the Japan Tobacco International (JTI Group of Companies), boasts a rich history that reflects the way the country itself has transformed over the past half a century.


The Company started as East African Tobacco, with the factory officially being opened by Mwalimu Julius K. Nyerere on December 4, 1961.

In 1967, the Company underwent nationalization with the Government of Tanzania acquiring 60% stake from British American Tobacco.


In 1975 the government acquired the remaining 40%. The Company was renamed Tanzania Cigarette Company Limited (TCC). Fast forward to 1995, TCC was privatized and RJ Reynolds Tobacco of USA acquired a 51% stake in TCC.

In 1999, JT acquired all non-US Tobacco operations of RJ Reynolds Tobacco and consequently TCC. In 2000, TCC Plc was listed on the Dar es Salaam Stock Exchange. JTI, increased its shareholding in TCC Plc from 51% to 75%.

Today, TCC Plc shares a common aspiration with the nation for success and respect. The Company has nationwide operational coverage in Tanzania, with staff in 16 regions.



Historia Fupi



Historia Fupi

TCC Plc, ni kampuni tanzu ya Kampuni ya kimataifa ya Japan Tobacco International (JTI Group of Companies), TCC Plc inajivunia historia yake ya tangu kuanzishwa kwake ambayo inaakisi jinsi nchi ya Tanzania ilivyopiga hatua ya maendeleo katika kipindi cha zaidi ya nusu karne iliyopita.

Kampuni ilianzishwa kama East African Tobacco, na kiwanda kikafunguliwa rasmi na Mwalimu Julius K. Nyerere tarehe 4 Desemba, 1961.


Mnamo mwaka 1967, Serikali ya Tanzania ilitaifisha 60% kutoka Kampuni ya British American Tobacco.

Mwaka 1975, Serikali ilikabidhiwa 40% ya hisa zilizobaki na jina la Kampuni likabadilishwa na kuwa Kampuni ya

Sigara Tanzania (Tanzania Cigarette Company Limited). Mwaka 1995, TCC ilitabafishwa na RJ Reynolds Tobacco ya Marekani ilinunua 51% ya hisa za TCC.

Mwaka 1999, JT ilinunua operesheni zote za tumbaku za RJ Reynolds Tobacco zilizo nje ya Marekani, na hivyo kupata hisa za TCC. Mwaka 2000, TCC Plc iliorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na JTI iliongeza hisa zake kutoka 51% hadi 75%.

Mpaka sasa, TCC Plc inashiriki ndoto moja na Taifa kuelekea mafanikio na heshima. Shughuli za Kampuni zimeenea nchi nzima ikiwa na matawi na wafanyakazi katika mikoa 16.




The TCC Plc Value Chain

Research and Development (R&D) - Innovation and Product Development

Consumer Insights and Trends: R&D at JTI involve understanding consumer preferences and market trends, ensuring that the products meet evolving consumer demands and comply with health regulations.

Procurement / Sourcing High-Quality Tobacco

The procurement process involves sourcing high-quality tobacco leaves, which are essential for producing products. TCC Plc through the JTI global procurement office works with local and international tobacco players, focusing on sustainable and ethical sourcing practices. Effective supply chain management ensures a consistent and reliable supply of raw materials, which is crucial for maintaining production schedules and product quality.



Manufacturing - Production Efficiency

The manufacturing process at TCC Plc involves transforming lamina and stem into finished products. This includes blending/conditioning, cutting, drying, making and packing of cigarettes, with a focus on efficiency and quality control.

Compliance with Standards: Adhering to health, safety, and environmental standards is crucial. TCC Plc's manufacturing processes is designed to minimize waste and reduce environmental impact while ensuring product safety.

Marketing - Brand Development

Marketing strategies involve building and maintaining strong brand identities, crucial to attract and retain consumers.

Regulatory Compliance: Given the nature of tobacco products, TCC Plc's marketing efforts must comply with strict advertising and promotion regulations, focusing on responsible marketing practices.

Sales - Extensive Distribution Network

TCC Plc's distribution network is key to ensuring that products are available to consumers across various retail channels, including supermarkets, convenience stores, retail shops and specialized tobacco shops.

Sales Strategies: Sales strategies include direct sales, partnerships with retailers, and promotional campaigns to drive product uptake and customer loyalty.

Each of these stages in TCC Plc's value chain is interconnected, contributing to the Company's overall success. R&D drives innovation, procurement ensures quality raw materials, manufacturing turns these materials into products, marketing builds the brand and promotes the products, and sales ensure that these products reach and satisfy the consumers.


Mnyororo wa Thamani wa TCC Plc

Utafiti na Maendeleo (R&D) - Ubunifu na Maendeleo ya Bidhaa

Taarifa na mwelekeo wa matumizi ya bidhaa zetu kwa watumiaji: Utafiti na Maendeleo (R&D) kwa JTI unahusisha kuelewa matakwa ya watumiaji na mwenendo wa soko, ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinakidhi mahitaji ya watumiaji na kuzingatia kanuni za afya.

Manunuzi ya Tumbaku yenye Ubona wa Juu

Mchakato wa ununuzi huusisha kupata majani ya tumbaku yenye ubora wa hali ya juu, ambayo ni muhimu kwa kuzalisha bidhaa. TCC Plc kupitia ofisi ya ununuzi ya JTI inafanya kazi na wadau wa tumbaku wa ndani na wa kimataifa, kwa kuzingatia mbinu endelevu zenye weledi za kupata malighafi. Usimamizi wa mnyororo wa ugavi wenye ufanisi unahakikisha ugavi thabiti na wa kuaminika wa malighafi, ambao ni muhimu kwa kudumisha ratiba za uzalishaji na ubora wa bidhaa.



Uzalishaji - Ufanisi Katika Uzalishaji

Mchakato wa uzalishaji wa Kampuni ya TCC Plc unahusisha kuchakata majani ya tumbaku kuwa bidhaa zilizokamilika. Mchakato huu inajumuisha kuchanganya, kukata, kukau-sha, kutengeneza, na kupaki sigara, huku kukiwa na mkazo kwenye ufanisi na udhibiti wa ubora.

Kuzingatia Viwango: Kuzingatia viwango vya afya, usalama, na mazingira ni muhimu. Mchakato wa uzalishaji wa Kampuni umetengenezwa kupunguza taka na kupunguza athari za mazingira na kuhakikisha usalama wa bidhaa.

Masoko - Maendeleo ya Chapa za Bidhaa

Mikakati ya masoko huusisha ujenzi na ulinzi wa muonekano wa chapa za bidhaa, ambazo ni muhimu kuvutia na kudumisha watumiaji.

Kuzingatia Utii wa Sheria: Kwa kuzingatia asili ya bidhaa za tumbaku, jitihada za masoko za TCC Plc lazima ziendane na kuheshimu sheria kali za matangazo na kuzingatia mbinu za masoko zenye uwajibikaji

Mauzo - Mtandao Mpana wa Usambazaji

Mtandao wa TCC Plc wa usambazaji wa bidhaa ni muhimu katika kuhakikisha kuwa bidhaa zinapatikana kwa wateja kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na maduka makubwa, maduka ya rejareja, na maduka maalum ya tumbaku. Mbinu za mauzo: Mbinu za mauzo zinajumuisha mauzo ya moja kwa moja, ushirikiano na wuzaji wa rejareja, na matangazo ili kuongeza mauzo na uaminifu wa wateja.

Kila moja ya hatua hizi katika mnyororo wa thamani wa TCC Plc zimeunganishwa, zikichangia kwenye mafanikio ya jumla ya Kampuni. Utafiti na Maendeleo (R&D) ni idara inayoendesha ubunifu, manunuzi inahakikisha malighafi bora, uzalishaji inageuza malighafi hizi kuwa bidhaa, masoko inajenga chapa za bidhaa na kukuza bidhaa, na mauzo yana hakikisha bidhaa hizi zinafikia na kuridhisha watumiaji.

Product Portfolio

Orodha ya Bidhaa




Performance Review

TCC Plc has experienced an increased revenue growth of 9.7% for the year 2023 TZS 373,527 million (2022: TZS 340,604 million) and increase in gross profit by 6.9% 2023 TZS 204,097 million (2022: TZS 190,841 million). Despite 20% increase in excise tax and pressure on operating costs,

the Company managed to deliver a stable profit for the year 2023 TZS 99,083 million (2022: TZS 106,764 million). The Company also generated a positive increase in net cash flow of TZS 22,082 million (2022: TZS (6,522) million).

Produced and Sold Quantities in 2023




Uhakiki wa Utendaji


Mwaka 2023, TCC Plc imepata ongezeko la ukuaji wa mapato kwa 9.7% na jumla ya mapato ya TZS 373,527 milioni (2022: TZS 340,604 milioni) na ongezeko la faida ghafi kwa 6.9% hadi TZS 204,097 milioni 2023 (2022: TZS 190,841 milioni). Pamoja na ongezeko la 20% kwenye kodi ya ushuru wa forodha na gharama za uendeshaji,

Kampuni imeweza kutengeneza faida kwa mwaka 2023 ya TZS 99,083 milioni (2022: TZS 106,764 milioni). Pia, Kampuni ilitengeneza ongezeko chanya la mzunguko halisi wa fedha wa TZS 22,082 milioni (2022: TZS 6,522 milioni).

Kiasi kilichozalishwa na kilichouzwa kwa mwaka 2023




Key Performance Indicators




Revenue

Numbers displayed in TZS Million




Profit Margin




Gross Profit

Numbers displayed in TZS Million




Dividend Per Share

Numbers displayed in TZS



Net Cash Flow From Operating Activities

Numbers displayed in TZS Million



Viashiria Muhimu vya Utendaji



373,527

katika Milioni za TZS

Mapato



27%

kwa %

Kiwango cha Faida



204,097

katika Milioni za TZS

Faida ya Jumla



500

TZS

Gawio kwa kila Hisa




82,452

katika Milioni za TZS


Mzunguko wa Fedha wa Uendeshaji

Mapato

Takwimu zinaonyeshwa katika Milioni za TZS




Kiwango cha Faida




Faida ya Jumla

Takwimu zinaonyeshwa katika Milioni za TZS




Gawio kwa kila Hisa

Takwimu zinaonyeshwa katika TZS



Ongezeko/Punguzo halisi la Mzunguko wa Fedha kwa Mwaka kutokana na Shughuli za Uzalishaji

Takwimu zinaonyeshwa katika Milioni za TZS



Members of the Board

Wajumbe wa Bodi



Mr. Paul D. Makanza

Board Chairman

First appointed as Chairperson of TCC Plc Board on August 3, 2017. Re-elected in the same position on August 11, 2023

- Mr. Makanza has two decades of senior-level management experience in various roles. He currently serves as Chairman of several esteemed other boards: Confederation of Tanzania Industries (CTI), Tanzania Start-up Association (TSA) and ABSA Bank Tanzania Limited. He also acts as Vice-Chairman in the board of Tanzania Private Sector Foundation (TPSF), Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC) and as board member of the East African Business Council.
- His expertise lies in finance, strategy, corporate governance, and advocacy, making him a respected figure in both private and public sectors. Throughout his career he has remained committed to excellence and has contributed significantly to the organizations and industries he has been involved with. Prior to his current roles, he gained valuable experience at JTI Tanzania (TCC Plc), JTI UK, and PricewaterhouseCoopers (PwC) Tanzania.

Mweyekiti wa Bodi

Aliteuliwa kwa mara ya kwanza kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya TCC Plc tarehe 3 Agosti, 2017. Akateuliwa tena kwenye nafasi hiyo kwa awamu nyingine tarehe 11 Agosti 2023

- *Mr. Makanza ana uzoefu wa zaidi ya miongo miwili katika uongozi wa juu kwenye nafasi tofauti. Kwa sasa anahudumu kama mwenyekiti wa bodi zingine zifuatazo: Shirikisho la Viwanda Tanzania, Umoja wa Biashara Fadhilishi, na Benki ya ABSA Tanzania. Pia ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Mjumbe wa Bodi ya Baraza la Biashara la Afrika Mashariki.*
- *Ni mtaalamu aliyebobea katika maswala yanayohusu fedha, mikakati na utawala, uwakilishi na utetezi. Mambo yanayomfanya kuwa mtu anayeheshimika katika sekta binafsi na umma. Katika safari yake ya kikazi, amechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya mashirika na sekta ambazo amefanya kazi akitimiza wajibu wake kikamilifu katika kipindi chake chote cha utumishi. Kabla ya majukumu yake ya sasa, alipata uzoefu mkubwa katika majukumu yake ndani ya JTI Tanzania (TCC Plc), JTI UK, na PricewaterhouseCoopers (PwC) Tanzania.*



Mr. Bakari Mbaruku Makulo

Appointed to the TCC Plc Board on January 01, 2023, as a nominee of the Government of the United Republic of Tanzania representing minority shareholders.

- Prior to his retirement he served as: Vocational Education and Training Authority (VETA) Regional Director central zone based in Dodoma (2014 - 2016), VETA Zonal vocational training centers coordinator for central zone (2008-2013), VETA Zonal vocational training centers coordinator for lake zone (2001- 2008), and prior to 2001 he was an academician in several institutions.

Alichaguliwa kwenye Bodi ya TCC Plc tarehe 01 Januari, 2023, kama mteule wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwakilisha wanahisa wenye hisa chini ya nusu ya hisa zote.

- *Kabla ya kustaafu alihudumu kama: Mkurugenzi wa Kanda wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) katika kanda ya kati iliyoko Dodoma (2014 - 2016), Mratibu wa vituo vya mafunzo ya Ufundi Stadi vya kikanda vya VETA kwa kanda ya kati (2008-2013), Mratibu wa vituo vya mafunzo ya Ufundi Stadi vya kikanda vya VETA kwa kanda ya ziwa (2001 - 2008) na Kabla ya mwaka 2001, alikuwa mwanazuoni katika taasisi mbalimbali.*



Mr. Johnny Ng

Appointed to the TCC Plc Board on January 1, 2021.

- Currently JTI Finance Vice President, Asia Pacific region from 2022.
- Previous roles within JTI include: Internal Audit Vice President of JT International SA from 2019 until his current appointment, CFO and Vice President of JTI Russia (2016 - 2019), JTI Finance Vice President Taiwan (2005-2016), and Finance Director JTI China (2002- 2005). Before joining JTI he worked as Senior Consultant - Deloitte Consulting Hong Kong (2000-2002), Business Analyst with PwC Limited Hong Kong (1998 to 1999), International Consultant - HSO Business System China Limited in Hong Kong (1997- 1998) and he holds a Master of Business Administration.

Aliteuliwa kwenye Bodi ya TCC Plc tarehe 1 Januari, 2021

- *Kwa sasa ni Makamu wa Rais wa Fedha wa JTI, eneo la Asia Pacific.*
- *Nafasi zake za awali zinajumuisha: Makamu wa Rais wa Ukaguzi wa Ndani wa JT International SA kuanzia mwaka 2019 hadi uteuzi wake wa sasa, CFO na Makamu wa Rais wa JTI Urusi (2016 - 2019), Makamu wa Rais wa Fedha wa JTI Taiwan (2005-2016), Mkurugenzi wa Fedha wa JTI China (2002- 2005). Kabla ya kujiunga na JTI, nafasi mbalimbali alizoshikilia zilijumuisha: Mshauri Mwandamizi - Deloitte Consulting Hong Kong (2000-2002), Mchambuzi wa Biashara katika PwC Limited Hong Kong (1998 - 1999) na Mshauri wa Kimataifa - HSO Business System China Limited huko Hong Kong (1997- 1998). Ana Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara.*



Mr. Onesmo Makombe

Appointed to the TCC Plc Board on April 23, 2021, representing minority shareholders.

- Currently Mr. Makombe is the Head of Financial Consumer Protection Department at the Bank of Tanzania (BOT), a role served from 2022.
- Previous roles in public service include: Commissioner and Chief Executive Officer of the Financial Intelligence Unit (FIU) (2015 to 2021), Chair of the Eastern and Southern Anti-Money Laundering Group (ESAAMLG) Task Force (2017- 2018), Acting Commissioner FIU (2013), Assistant Commissioner FIU (2011), Financial and Intelligence Analyst under the Ministry of Finance (2007-2011), Bank Examiner with the Bank of Tanzania (BoT) (1997-2007).

Aliteuliwa kwenye Bodi ya TCC Plc tarehe 23 Aprili, 2021, akiwakilisha kundi la wanahisa wenye hisa chini ya nusu ya hisa zote

- *Kwa sasa Mr. Makombe ni Mkuu wa Idara ya Ulinzi wa Mlaji katika Benki Kuu ya Tanzania (BOT), nafasi ambayo ameitumikia kuanzia 2022.*
- *Nafasi za awali katika utumishi wa umma zinajumuisha: Kamishna na Afisa Mtendaji Mkuu wa Kitengo cha Upelelezi wa Fedha (FIU) (2015 - 2021), Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Kupambana na Utakatishaji Fedha ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAAMLG) (2017- 2018), Kamishna mkuu wa mpito FIU (2013), Kamishna Msaidizi FIU (2011), Mchambuzi wa Fedha na Upelelezi chini ya Wizara ya Fedha (2007-2011), Mkaguzi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) (1997-2007).*



Mr. Bertrand Tamisier

Appointed to the TCC Plc Board of Directors on January 01, 2018, and re-appointed on January 01, 2021.

- Chief Financial Officer (CFO) and Vice President of JTI Middle East, Near East, Africa, Turkey (MENEAT) & Global Travel Retail (GTR) Region since January 2018.
- Over 25 years of extensive experience in finance within JTI. Previous roles within JTI include: Global Financial Operations VP (2017), Strategy and Insights Lead VP (2016-2017), CFO and VP in JTI SA and Central Europe Region (2008-2011 and 2011-2016), Adriatica CFO (2007-2008), Senta Integration Director (2006-2007), Research and Development Scientific and Regulatory Affairs Finance Director (2005 – 2006), CFO and Finance Director in Iran (2002-2005), World Wide Duty Free (WWDF) & MENA Finance Controller (2000- 2002), Baltics, Belarus and Kaliningrad CFO (1998- 1999) and CIS Finance Manager Operations and Exports (1997-1998).

Aliteuliwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya TCC Plc tarehe 01 Januari, 2018, na kuteuliwa tena tarehe 01 Januari, 2021.

- *Afisa Mkuu wa Fedha (CFO) na Makamu wa Rais wa JTI Mashariki ya Kati, Mashariki ya Karibu Afrika, Uturuki (MENEAT) & Eneo la Biashara ya Usafiri wa Kimataifa (GTR) tangu Januari 2018.*
- *Ana uzoefu mkubwa katika maswala ya fedha ndani ya JTI kwa zaidi ya miaka 25. Alihudumu kama: Makamu wa Rais wa Operesheni Fedha za Kimataifa (2017), Makamu wa Rais wa Mikakati na Maarifa (2016-2017), Afisa Mkuu wa Fedha na Makamu wa Rais katika JTI SA na eneo la Ulaya ya Kati (2008-2011 na 2011-2016), Mkurugenzi mtendaji wa Fedha wa Adriatica (2007-2008), Mkurugenzi wa Senta Intergation (2006-2007), Mkurugenzi wa Fedha anayesimamia maswala ya Utafiti, Ukuzaji/Mkurugenzi wa Maswala ya Kitafiti Kisayansi, Sheria, na Fedha nchini Iran (2002 – 2005), Mdhiti Fedha wa WWDF & MENA, Mkurugenzi wa Fedha wa Baltics, Belarus and Kaliningrad na Maneja wa Fedha na operesheni na mauzo ya nje wa CIS.*



Mr. Takashi Araki

General Manager and Chief Executive Officer (CEO) of TCC Plc.

First appointed as Director of TCC Plc on October 1, 2022.

- 30 years of experience in various leadership positions within the JT Group with increasing responsibility.
- Prior to joining TCC Plc, he worked as Corporate Business Development & Corporate Strategy Vice President of the JT Group, based in Japan

Meneja Mkuu na Afisa Mtendaji Mkuu wa TCC Plc.

Aliteuliwa kwa mara ya kwanza kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TCC Plc tarehe 1 Oktoba, 2022.

- *Miaka 30 ya uzoefu katika nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya Kampuni mama JT Group.*
- *Kabla ya kupewa nafasi hii, alihusika na usimamizi wa maendeleo ya biashara na mikakati katika JT Group, yenye makao yake makuu nchini Japani.*



Ms. Sevgi Denge Mc Neill

Appointed to the TCC Plc Board of Directors on January 01, 2024.

- Currently Ms Mc Neill is the JTI Regional Finance Vice President for MENEAT as of January 2024.
- Previous roles at JTI included: JTI Corporate Strategy Director (2020-2024), Finance Director Turkey (2018 - 2020), JTI HQ Geneva's Global Finance Transformation Director (2017 - 2018), Global Functions Finance Director (2014 – 2017), Global Leaf Finance Operations Director (2011 – 2014), Global Supply Chain Finance Director (2009 – 2011), Project Management Office Lead (2006 – 2008), Global IT Finance Controller (2004 – 2006), JTI Turkey's Process Improvement Manager (2003 – 2004), JTI Turkey's Financial Planning and Analysis Manager (2000 – 2003) and JTI Turkey's Accounting (1998 – 1999).

Ameteuliwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya TCC Plc tarehe 01 Januari, 2024.

- *Kwa sasa Ms Mc Neill ni Makamu wa Rais wa Fedha wa Kikanda wa JTI kwa MENEAT kuanzia Januari 2024.*
- *Majukumu ya awali katika JTI yalijumuisha: Mkurugenzi wa Mikakati wa Kampuni JTI (2020-2024), Mkurugenzi wa Fedha Uturuki (2018 - 2020), Mkurugenzi wa Mabadiliko ya Fedha Kimataifa katika Makao Makuu ya JTI Geneva (2017 - 2018), Mkurugenzi wa Idara za Fedha Kimataifa (2014 – 2017), Mkurugenzi wa Shughuli za Kifedha Upande wa Ununuzi wa Tambaku (2011 – 2014), Mkurugenzi wa Fedha GSC (2009 – 2011), Kiongozi wa ofisi ya usimamaizi wa miradi (2006-2008), Mhasibu Mkuu wa Fedha - teknolojia Kimataifa (2004 – 2006), Meneja wa Mipango ya Fedha na Uchambuzi wa JTI Uturuki (2000 – 2003), Meneja wa Mipango ya Fedha na Uchambuzi wa JTI Uturuki (2000 – 2003) na Uhasibu JTI Uturuki (1998 – 1999).*



Ms. Biljana Ivosevic

Appointed to the TCC Plc Board of Directors on January 01, 2024.

- Currently Ms. Ivosevic is the Finance Director for JTI Dutch Holdings since 2022.
- Her previous roles were JTI Regional Tax Director EE & Americas in 2020, JTI Regional Tax Director WE & Americas (2018 - 2020), Tax Director JTI SA (2016 - 2018), Indirect Tax Director JTI SA (2014 - 2016), JTI SA Controlling and Reporting Manager (2012 – 2014) and Finance Controller Adriatica (2008 -2012). Before joining JTI, she worked at Coca Cola Hellenic Bottling Company Serbia and British American Tobacco (BAT) Serbia in different finance positions.

Ameteuliwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya TCC Plc tarehe 01 Januari, 2024.

- *Kwa sasa Ms. Ivosevic ni Mkurugenzi wa Fedha JTI Dutch Holdings tangu 2022.*
- *Majukumu ya awali yalikuwa: Mkurugenzi wa Kodi wa Kikanda wa JTI EE & Amerika mwaka 2020, Mkurugenzi wa Kodi wa Kikanda wa JTI WE & Amerika (2018 - 2020), Mkurugenzi wa Kodi JTI SA (2016 - 2018), Mkurugenzi wa Kodi zisizo za Moja Kwa Moja JTI SA (2014 - 2016), Meneja wa Udhhibiti na Ripoti wa JTI SA (2012 – 2014) na Mhasibu Mkuu Adriatica (2008 -2012). Kabla ya kujiunga na JTI, alifanya kazi katika Kampuni ya Uuzwaji wa vinywaji baridi ya Coca Cola Hellenic Serbia na British American Tobacco (BAT) Serbia katika nafasi mbalimbali za fedha.*

Management Team Timu ya Usimamizi



Takashi Araki

General Manager and CEO
Meneja Mkuu na Afisa Mtendaji Mkuu



Samwel Mandara

Manufacturing Director
Mkurugenzi wa Uzalishaji



Thomas Hadorn

Finance Director
Mkurugenzi wa Fedha



Yassin Hussein

Marketing Director
Mkurugenzi wa Msaikoti



Patricia Mhondo

Corporate Affairs and Communication Director
Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano ya Kampuni



Angela Mangecha

People and Culture Director
Mkurugenzi wa Watu na Utamaduni




Godson Killiza

Legal Affairs Director
Mkurugenzi wa Maswala ya Sheria



Lucas Mwamanenge

Sales Director
Mkurugenzi wa Mauzo



03

MESSAGE TO STAKEHOLDERS UJUMBE KWA WADAU



Message from the Chairman

Dear Esteemed Shareholders and Stakeholders,

A Reflection on 2023

On behalf of the TCC Plc Board of Directors, I am pleased to present an overview of TCC Plc's performance for the year ending December 31, 2023. Our enduring commitment to sustainable growth and responsible corporate stewardship has remained steadfast throughout the year.

Guided by our overarching purpose of "Creating fulfilling moments. Creating a better future," we have stayed true to our core principles, ensuring that we consistently prioritize and exceed the expectations of our valued consumers, shareholders, employees, and the broader society. Our core values of fostering a winning attitude, collaboration as 'One Team,' a commitment to quality, and responsible behaviour have been pivotal in driving our strategic endeavours forward.

Financial Achievements

Our collective efforts in 2023 delivered another year of remarkable achievements across both financial and non-financial metrics and broader strategic initiatives.

Revenue grew 9.7% year-on-year to TZS 373,527 million, driven by a robust 11% domestic and export volume growth. Furthermore, strategic pricing adjustments to our premium brands in response to a 20% excise tax hike in June 2023 also contributed to our revenue growth.

Although our profit figures declined marginally, reflecting the dynamic nature of our business landscape, we maintained a resilient financial performance. Our profit before tax (PBT) experienced a modest decline of 7.2% to TZS 99,083 million, and our net profit after tax (PAT) for the year decreased marginally by 4.2% to TZS 66,233 million. Rising costs across different areas of our business affected our bottom line, notably a 13.1% increase in the cost of goods sold due to higher costs of imported raw materials, elevated transportation and logistics costs due to higher fuel costs and increased recharges.

Going forward, we remain committed to addressing cost pressures while seizing growth opportunities in our target markets. Our focus remains on prudent financial management, which aims to foster sustainable value creation for our esteemed shareholders.

Delivering Stakeholders' Value

TCC Plc actively creates long-term sustainable value for our key stakeholders through two core avenues: corporate value and social value. We prioritize enhancing shareholder returns while contributing to society's sustainable development through our business activities, recognizing both aspects as equally important.

Beyond Profit: Our Commitment to Social Responsibility

Our sustainability strategy is built upon three key pillars: product and service, people (safety, community investment, employer of choice), and regulatory engagement.

Regarding products and services, we aim to provide consumers with an expanded range of high-quality and innovative products. Notably, we enhanced our product portfolio with the introduction of Winston Expand in July 2023.

In our people pillar, safety continued to be an integral part of our operations and a priority in everything we do, with a key focus on employees' ownership and behavioural change. Our community investment initiatives benefited over 1,700 community members, with employees contributing 360 collective hours. Additionally, for the 6th consecutive year, the Global Top Employer Institute recognized us as an employer of choice, praising our talent management, empowerment practices, and diversity efforts. Moreover, we increased female workforce participation to 21.2%, up from 20% in 2022, aligning with our goal of reaching a 30% female workforce by 2030. In supply chain management, we reduced greenhouse gas emissions by 4% and waste generation by 50%.

On regulatory engagement, we actively engaged policy and decision-makers for fair and balanced regulations and collaborated with government agencies to combat illicit trade in tobacco products. These endeavours reaffirm our commitment to sustainable and responsible practices.

Dividends and Growth Opportunities

With a robust net profit and free cash flow, the TCC Plc Board of Directors proposed a final ordinary dividend payment of TZS 200 per share for the fiscal year ending December 31,

2023. Coupled with the interim ordinary dividend of TZS 300 per share paid to shareholders in June 2023, this brings the total ordinary dividend for the year to TZS 500 per share. Distribution of dividend at a level of 76% of net profits provides a competitive level of return to our shareholders whilst also allowing reinvestment for future growth potential to which we can remain committed.

The final ordinary dividend, subject to shareholders' approval at the Annual General Meeting of Shareholders in April 2024, will be paid in May 2024.

Looking Ahead to 2024

Looking ahead to 2024, I am optimistic about TCC Plc's business outlook despite prevailing global economic uncertainties, including geopolitical tensions.

In Mainland Tanzania, growth is projected to remain robust, with a forecasted GDP growth rate of 5.2% in the first quarter of 2024. The inflation outlook is also favourable, with forecasts indicating a low inflation rate of around 3.2%, well below the 5% target.

Furthermore, we are encouraged by the continued improvement of Tanzania's business environment and investment climate. However, we remain mindful of external risks, such as geopolitical tensions, which could impact the cost of imported goods.

Nevertheless, with our solid strategy and execution capabilities, we are well-positioned to navigate challenges and capitalize on emerging opportunities.

Appreciation

I extend heartfelt appreciation to our stakeholders for their unwavering support. Special thanks to our parent company, JTI, our dedicated management and employees, the Government and its agencies, and business associations for their invaluable assistance throughout 2023. Together, we look forward to pursuing our shared goals.

Sincerely,

Paul Makanza
Chairman of the Board, TCC Plc



Ujumbe kutoka kwa Mwenyekiti

Ndugu Wanahisa na Wadau.

Tafakari ya Mwaka 2023

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya TCC Plc, ninayo furaha kuwasilisha muhtasari wa utendaji wa TCC Plc kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2023. Juhudi na kujitoa kwetu katika uwajibikaji na ukuaji endelevu wa biashara ziliendelea kuba kua thabiti kwa mwaka mzima.

Tukiwa tunaongozwa na dhumuni letu la "Kutengeneza Nyakati za Furaha. Kutengeneza Kesho iliyo Bora Zaidi." tumebaki waaminifu katika kanuni zetu za msingi, tukihakikisha kwamba tunavipa kipaumbele na kuzidi kutimiza matarajio ya watumiaji wa bidhaa zetu, wanahisa, wafanyakazi, na jamii kwa ujumla. Maadili yetu ya msingi ya kukuza mtazamo wa ushindi, ushirikiano kama 'Timu Moja,' ahadi ya kuzingatia ubora, na mwenendo wa uwajibikaji yamekuwa muhimu katika kusukuma mbele juhudi zetu za kimkakati.

Mafanikio ya Kifedha

Juhudi zetu za pamoja katika mwaka wa 2023 zilileta mwaka mwingine wa mafanikio ya kipekee katika nyanja za kifedha na zisizo za kifedha pamoja na mipango mikubwa ya kimkakati.

Mapato yaliongezeka kwa 9.7% mpaka kufikia TZS 373,527 milioni, yakichochea na ukuaji imara wa 11% wa mauzoya soko la ndani na la nje. Zaidi ya hayo, marekebisho ya kimkakati ya bei kwenye bidhaa zetu za daraja la juu yaliyotokana na ongezeko la ushuru wa bidhaa wa 20% mwezi Juni 2023 pia yalichangia katika ukuaji wa mapato yetu.

Ingawa takwimu zetu za faida zilipungua kidogo, kutokana na mabadiliko ya mazingira yetu ya biashara, lakini tulidhibiti utendaji thabiti wa kifedha. Faida yetu kabla ya kodi (PBT) ilipungua kwa kiasi kidogo cha 7.2% hadi kufikia TZS 99,083 milioni, na faida yetu halisi baada ya kodi (PAT) kwa mwaka ilipungua kwa 4.2% hadi kufikia TZS 66,233 milioni. Ongezeko la gharama katika maeneo mbalimbali ya biashara yetu lilikua na athari, hasa ongezeko la 13.1% katika gharama ya bidhaa zilizouzwa kutokana na gharama kubwa zaidi za malighafi zilizoagizwa kutoka nje, gharama kubwa za usafirishaji kutokana na ongezeko la gharama za mafuta na ongezeko la malipo ya huduma.

Tumejidhatiti kuendelea kushughulikia shinikizo linalotokana na ongezeko la gharama za kiuendeshaji huku tukitafuta fursa za ukuaji zilizopo katika masoko yetu lengwa kadri tunavyozidi kusonga mbele. Kipaumbele chetu kitaendelea kuwa kwenye usimamizi makini wa fedha, ambao unalenga kuongeza thamani endelevu kwa wanahisa wetu wapendwa.

Kuleta Thamani kwa Wadau

TCC Plc inalenga kujenga thamani endelevu ya muda mrefu kwa wadau wetu muhimu kupitia njia mbili kuu: thamani ya Kampuni na thamani ya kijamii. Tunaweka kipaumbele katika kuimarisha mapato ya wanahisa wakati tunachangia maendeleo endelevu ya jamii kupitia shughuli zetu za biashara, tukitambua kuwa vyote ni muhimu.

Zaidi ya Faida: ahadi yetu ya kuwajibika kwenye jamii

Mkakati wetu endelevu unajengwa katika nguzo kuu tatu bidhaa na huduma, watu (usalama, uwekezaji katika jamii, mwajiri bora), na ushirikiano na wasimamizi wa sheria.

Kuhusu bidhaa na huduma, lengo letu ni kuwapa watumiaji wetu bidhaa mbalimbali zenye ubora na ubunifu. Pia, tumengeza bidhaa mpya kwa kuingiza Winston Expand mwezi Julai 2023.

Katika nguzo yetu ya watu, usalama umeendelea kuwa sehemu muhimu ya shughuli zetu na kipaumbele katika kila tunachofanya, tukizingatia umiliki na mabadiliko ya tabia za wafanyakazi. Miradi yetu ya uwekezaji kwa jamii imenufaisha zaidi ya wanajamii 1,700, na wafanyakazi wakichangia jumla ya masaa 360. Aidha, kwa mara ya sita mfululizo, taasisi ya Global Top Employer imetutambua kama mwajiri bora, hasa katika usimamizi wa vipaji, uwezesaji, na juhudi za kuwa na mfumo unaojumuisha watu kutoka jamii tofauti. Zaidi ya hayo, tumeweza kuongeza ushiriki wa wanawake katika nguvu kazi hadi asilimia 21.2%, kutoka 20% mwaka 2022, tukilenga kufikia asilimia 30% ya nguvu kazi ya wanawake ifikapo mwaka 2030. Katika usimamizi wa mnyororo wa thamani, tumepunguza uzalishaji wa gesi chafu kwa 4% na uzalishaji wa taka kwa 50%.

Kuhusu ushirikiano na wadau wanaosimamia sheria, tulishirikiana kikamilifu na watengeneza sera na watoa maamuzi ili kupata sheria zenye kuchochea haki na usawa, na tukashirikiana na mashirika ya serikali kupambana na biashara haramu ya bidhaa za tumbaku. Jitihada hizi zinathibitisha dhamira yetu ya kudumisha mbinu endelevu na zenye uwajibikaji.

Gawio na Fursa za Ukuaji

Bodi ya Wakurugenzi ya TCC Plc ilipendekeza malipo ya gawio la mwisho la kawaida la TZS 200 kwa kila hisa kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2023. Pamoja na

gawio la kawaida la kati la TZS 300 kwa kila hisa lililolipwa kwa wanahisa mwezi Juni 2023, hii inafikisha jumla ya gawio la kawaida kwa mwaka huo kufikia TZS 500 kwa kila hisa. Utoaji wa gawio wa kiwango cha 76% ya faida halisi unaonesha ushindani wa urejeshaji wa faida kwa wanahisa wetu huku pia ukiwawezesha kudumu kwenye uwekezaji upya kwa ajili ya ukuaji wa baadaye.

Gawio la mwisho la kawaida, ambalo litatokana na idhini ya wanahisa katika Mkutano Mkuu wa Wanahisa mwezi Aprili 2024, litalipwa mwezi Mei 2024.

Matazamio kwa Mwaka 2024

Ninapoangalia mwaka 2024, nina matumaini makubwa kuhusu mwenendo wa biashara ya TCC Plc japokua kuna changamoto za kiuchumi ulimwenguni, na mivutano ya kisiasa inayoendelea.

